REDD net

Networking for equity in forest climate policy

KUANDAA NA KUTEKELEZA TAADHARI ZA MKUHUMI+ KATIKA NGAZI YA TAIFA KATIKA AFRIKA MASHARIKI

Na David M. Mwayafu & James W. Kisekka

2012

Acknowledgements

The authors would like to thank Emily Brickell for her valuable comments on the draft of this paper and presenters at the workshop in Nairobi: Mr. Robert Nabanyumya, Rahima Njaidi, Erneus Kaijage, Mary Sway, Xavier Mugumya, Emily Brickell, and all the workshop participants who gave insights on the direction of this paper.

Disclaimer

This paper is published by the REDD-net programme, supported by the Norwegian Agency for Development Cooperation (NORAD). The views and recommendations expressed in this paper are those of the authors and do not necessarily represent the views of the funders or institutions involved in REDD-net.

ABOUT REDD-NET

REDD-net is an international knowledge forum for southern civil society organizations through which they can access information about efforts to Reduce Emissions from Deforestation and forest Degradation, share their own experiences and help to build pro-poor REDD projects and policies. REDD-net is a partnership between Centro Agrononómico Tropical de Investigación y Enseñanza (CATIE), the Overseas Development Institute, RECOFTC - The Center for People and Forests and Uganda Coalition for Sustainable Development. REDD-net is funded by Norad.

For information about REDD-net contact William McFarland at ODI (w.mcfarland@odi.org.uk or visit **www.redd-net.org**
For more information about REDD-net East Africa and this paper, contact David Mwayafu (dmwayafu@ugandacoalition.or.ug)

Contents

UTANGULIZI i

1. HALI NA MAENDELEO YA TAADHARI ZA MKUHUMI+ 1

Mfumo wa Taadhari za MKUHUMI+ za Benki ya Dunia 2

Taadhari za MKUHUMI+ za Mkakati wa Umoja wa Mataifa Juu ya mabadiliko ya Hali ya Tabia Nchi (UNFCCC) 3

Viwango vya Mazingira, Jamii na Bioanuwai 3

Mifumo mingine ya Taadhari za MKUHUMI+ 4

2. UTEKELEZAJI WA TAADHALI ZA MKUHUMI+ KATIKA AFRIKA MASHARIKI 5

Sera Zilizopo na Maendeleo yaliyofikiwa 5

Tanzania 5

Uganda 6

Kenya 7

3. KUFANIKISHA TAADHARI ZA MKUHUMI+ KATIKA AFRIKA MASHARIKI 9

Miongozo kutoka kwa Washiriki katika Warsha juu ya Masuala ya Taadhari za MKUHUMI+ 9

4. HITIMISHO 11

References 12

UTANGULIZI

Wakati shughuli za MKUHUMI+ zina uwezo wa kuleta faida nyingi za kijamii na kimazingira, lakini pia kuna uwezekano wa shughuli hizo kuathiri mazingira pamoja na baadhi wa wadau, hasa zile jamii ambazo maisha yake yanategemea zaidi misitu. Uwezekano huu umesababisha mjadala maalum, hasa miongoni mwa jamii na mashirika ya kiraia. Hali kadhalika, uwezekano huu umesababisha swala la uhitaji wa juhudi za makusudi za kushughulikia masuala ya kijamii na mazingira yanayohusiana na mipango ya MKUHUMI+ lichukue sura maalum na kipaumbele katika ngazi za kimataifa, kitaifa na kijamii. Kwa mfano, katika mkutano wa umoja wa mataifa wa mwaka 2010 uliofanyika Cancun, serikali za mataifa mbalimbali zilikubaliana juu ya mfumo wa taadhari ambazo zinapaswa kuandaliwa na kutekelezwa katika mipango ya MKUHUMI+ (UNFCCC, 2010:). Pia, taasisi nyingi za kimataifa zimeandaa sera na taadhari mbalimbali za kimazingira na kijamii "ili kusaidia kutambua na kupunguza uwezekano wa shughuli zao kusababisha madhara kwa watu pamoja na mazingira.

Neno taadhari limekuwa na maana na kusudi tofauti miongoni mwa wadau mbali mbali kama vile serikali, wafadhili wahisani, wawekezaji, taasisi za kimataifa, jamii wazawa na tegemezi kwenye misitu, sekta binafsi, pamoja na za kiraia (Moss et al 2011). Zaidi ya hayo, majina mengine mbalimbali yamekuwa yakitumika kumaanisha neno taadhari. Haya ni kama vile, kanuni, viwango, vigezo, mikakati ya kukabiliana na hathari, tathmini za kimkakati za jamii na mazingira, pamoja na kanuni za tahadhari. Pamoja na tofauti katika majina/maneno haya yote, lengo kubwa la msingi katika haya yote ni kuzuia na kupunguza madhara yasiyofaa kwa watu na mazingira yao na badala yake kuhakikisha faida zinapatikana katika mchakato huu. .

Kihalisia zaidi, taratibu na sera za taadhari zinaandaliwa ili kuzuia, kukinga na kupunguza athari mbaya ya kijamii na kimazingira zitokanazo na miradi na mikakati, na pia ili kuweza kutekeleza mikakati ya kitaifa ambayo ina matokeo chanya kwa watu na mazingira. Kwa mfano nchi zinzaotekeleza miradi ya MKUHUMI+ zina sifa na historia kubwa ya rushwa (Benki ya Dunia, 2011) na uwezo mdogo wa kuzuia madhara yatokanayo na uwekezaji katika shughuli za kimaendeleo (Benki ya Dunia, 2005). Ujio wa pesa nyingi za MKUHUMI+ unaweza kuzidisha changamoto hizi za kiutawala. Hata hivyo ukuzaji na umiliki wa taadhari hizi kwa nchi husika unaweza kusaidia kuimarisha sheria za nchi husika na taasisi zake jambo ambalo linaweza kupelekea upatikanaji wa maendeleo endelevu. Uanzishaji wa viwango vya kijamii na kimazingira vinavyotambulika kimataifa kwa ajili ya kuongoza sera za kitaifa na miradi ya MKUHUMI+ ni dhana muhimu katika kuhakikisha ufanisi na matokeo ya usawa miongoni mwa jamii namazingira (Jagger et al., 2012).

1 MKUHUMI+ ni Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Mazingira Katika nchi zinazoendelea. Kulingana na Makubaliano ya mkutano wa Cancun mwaka 2010, MKUHUMI+ (unajumuisha vipengele 5 ambavyo ni Ufyekaji wa miti, Uharibifu wa misitu, Uhifadhi wa misitu, Usimamizi endelevu wa misitu,na Ukuzaji wa stock ya Kaboni ya misitu. Vipenge vyote hivi kwa pamoja vinafanya neno MKUHUMI+ liwe na alama ya (+), yaani MKUHUMI+ au 'REDD+'

© Adrian Paul Nel

1. HALI NA MAENDELEO YA TAADHARI ZA MKUHUMI+

Katika nchi nyingi mijadala ya taadhiri bado iko katika hatua ya awali sana na inachukua sehemu ndogo ya mjadala mzima wa sera ya MKUHUMI+. Jitihada nyingi za maandalizi na utayari wa MKUHUMI+ zimejikita zaidi juu ya maswala ya upimaji, ufuatiliaji na udhibitishaji wa Kaboni (MRV) na zimeyapa kipaumbele kidogo masuala ya msingi yanayohusiana na taadhari za MKUHUMI+(Jagger et al., 2012). Ripoti ya Kirk Herbertson wa international Rivers ioinaonyesha kwamba zaidi ya taasisi kumi na tano za kimataifa (Jedwali 1) zimejitahidi kufanya mabadiliko katika taadhari zake tangu 2008, na kwa sasa, walau taasisi nane ziko katika mchakato wa kubadilisha sera zake za zamani au kuandaa sera mpya kabisa. Kwa mujibu wa Herbertson (2012), taasisi za kibenki za maendeleo ndizo zenye mifumo mizuri ya taadhari ambayo ina taratibu za kina, na pia wafanyakazi wa taasisi hizo wana uzoefu wa miaka mingi katika maswala haya. Benki hizi, tangu 2008 zimafanya mabadiliko katika mifumo yao ya taadhari za MKUHUMI+.

Jedwali 1: Mabadiliko ya siku za karibuni katika baadhi ya taadhari

Taasisi	Hali /Mwaka wa mabadiliko
Benki ya Dunia	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Benki ya Maendeleo ya Africa	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Lugha katika majadiliano ya MKUHUMI+ katika ngazi ya UNFCCC	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Mfuko wa Kijani wa mabadiliko ya Tabia nchi	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Benki ya maendeleo ya Brazili, BNDES	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Mpago wa MKUHUMI+ wa Umoja wa Mataifa (UN-REDD)	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Kikundi cha usimamizi wa mazingira cha Umoja wa Maifata	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Mfuko wa mazingira wa Dunia (GEF)	Ziko katika mchakato wa kubadishwa
Ushirikiano wa kifedha wa Kimataifa (IFC)	Mabadiliko yalifanyika 2011
Mfuko wa kabooni ya misitu (FCPF)	Mabadiliko yalifanyika 2011
Kitengo cha maendeleo cha Ujerumani	Mabadiliko yalifanyika 2011
Benki ya maendedeleo ya Asia	Mabadiliko yalifanyika 2009
Mradi wa Uwekezaji katika Misitu (FIP)	Mabadiliko yalifanyika 2011
Benki ya Ulaya kwa ajili ya Ujenzi na Mandeleo	Mabadiliko yalifanyika 2008
Benki ya Uagizaji na Usambazaji ya China	Mabadiliko yalifanyika 2008

imechukuliwa kutoka kwa Herbertson 2012

Mfumo wa Taadhari za MKUHUMI+ za Benki ya Dunia

Benki ya Dunia, ambayo inasemekana kuwa taadhari madhubuti zaidi miongoni mwa taasisi za kijamii za kimataifa, (Herbertson, 2012), inazo sera kumi za taadhari pamoja na sera ya upatikanaji wa taarifa hizo ambayo huongoza Benki pamoja na nchi wakopaji katika utambuzi, maandalizi, na utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya dunia (Moss et al., 2011). Sera tano kati ya hizi: Tathmini ya Mazingira (OP / BP 4.01), Mazingira Asilia (OP / BP 4.04), Misitu (OP / BP 4.36), uamishwaji usio wa hiari (OP / BP 4.12), na ile ya Wananchi Wazawa (OP / BP 4.10) ndio sera muhimu zaidi katika majadiliano kuhusu masuala ya kijamii na kimazingira ndani ya MKUHUMI+ (Moss et al. 2011). Angalia sanduku namba 1 hapa chini ambalo linatoa mukhtasari wa sera hizi za taadhari. Sera hizi zinatumika katika miradi yote inayofadhiliwa na benki ya dunia kupitia miradi ya mfuko wa kaboni ya misitu (FCPF) pamoja na ule wa Mpango wa Uwekezaji katika misitu (FIP).

Hata hivyo, sera hizi zina mapungufu katika utumiaji wake katika michakato ya maandalizi na upangaji wa utayari wa MKUHUMI+ (Readiness)(Moss et al., 2011). Hii ni kwa sababu, maandalizi ya sera hizi yalilenga zaidi ufadhili wa miradi kuliko upangaji wa jumla wa kimkakati ambao ndo hasa asilia ya MKUHUMI+ ambayo inalenga kusaidia katika shughuli za uchambuzi na maandalizi ambayo yatazaa, kwa mfano, mkakati wa taifa wa MKUHUMI+.

Awamu ya utayari (Readiness) wa MKUHUMI+ inahitaji mpango wa kimkakati ili kuhakikisha uunganishaji

Sanduku namba 1: Taadhari za Jamii na Mazingira za Mfuko wa Benki ya Dunia wa FCPF

Tathimini ya Mazingira (OP 4.01) ulenga katika kuzuia, kukinga na kupunguza au kufidia athari mbaya za katika mazingira, lakini kwa kadri iwezekanavyo, taratibu za kukinga zinapendekezwa zaidi juu ya zile za kupunguza au kufidia. Inazingatia maswala ya jamii na mazingira ya mradi katika namna unganishi. Inazingatia mazingira (anga, maji na aridhi); afya na usalama wa binadamu; maswala ya jamii (kuhama kusikokuwa hiari, wenyeji na wadhawa na rasilimali asilia) pamoja na maswala mtambuka na yale kimazingira kidunia.

Mazingira asilia (OP 4.04) usisitiza kwamba uhifadhi wa mazingira ya asili, kama mojawapo ya taratibu za kuhifadhi na kuboresha mazingira, ni muhimu katika kuhakikisha maendeleo endelevu ya muda mrefu.

Misitu (OP 4.36) usisitiza kwamba usimamizi, uhifadhi, na maendeleo endelevu ya mifumo ikolojia ya misitu pamoja na rasilimali andamizi ni muhimu sana katika kufanikisha uondoaji wa kudumu wa umasikini pamoja na kufanikisha maendeleo endelevu, bila kujali kama rasilimali hizo ziko katika nchi yenye misitu mingi, rasimali chache au zile zilizoharibiwa. Lengo la sera hii ni kuwasaidia waazimaji kutumia vizuri mchango wa misitu katika uondoaji umasikini wa kudumu, kuunganisha vyema misitu katika ukuaji endelevu wa uchumi, pamoja na kuhifadhi huduma muhimu za kijamii na kimazingira zitokanazo na misitu. Kwa mfano, pale ambapo ni muhimu kuboresha misitu na kupanda miti kwa ajili ya kufanikisha malengo haya, benki uwasaidia wakopaji kufanikisha shughuli hizi ambazo uhifadhi na au kukuza bioanuai na kuboresha ufanisi wa hudama za mifumoikolojia. Benki pia uwasaidia wakopaji kuanzisha na kuendeleza mashamba ya miti ambayo ni rafiki wa mazingira, yenye manufaa kwa jamii na yenye faida za kiuchumi kwa ajili ya kusaidia kukidhi mahitaji yanayoongezeka hasa ya ya huduma na mazao ya misitu.

Kuhama kusikokuwa hiari (OP 4.12):Sera hii uzingatia kwamba kuhama kusikokuwa hiari kunaweza kusababisha matatizo mengi ya kudiumu, umasikini na uaharibifub wa mazingira isipokuwa tu pale ambapo hatua madhubuti zimeandaliwa na kutekelezwa kwa umakini zaidi.

Watu wenyeji na wazawa (OP 4.10): sera hii inalenga kuchangia katika mkakati wa Benki ya Dunia wa kuhakikisha uondoaji wa umasikini na kuleta maendeleo endelevu kwa kuhakikisha kwamba michakato ya maendeleo inaheshimu kikamilifu haki za binadamu,uchumi, na tamaduni za wenyeji na wazawa. Sera hii inasisitiza matumizi ya utaratibu wa kibali huru, awali, na taarifu ambacho (free, prior and informed consent) ambao unalenga kuhakikisha kukubalika kwa mradi miongoni mwa wanajamii walioathirika hasa wenyeji na wazawa. Sera hii usisitiza kwamba miradi yote inayofadhiliwa na benki ya dunia iandaliwe kwa namna ambayo itahakikisha kuwa wenyeji na wazawa wanapokea mapato ya kijamii na kiuchumi ambayo yanakubalika kijamii na pia yanazingatia maswala ya jinsia miongoni mwa vizazi.

wa masuala ya kijamii na kimazingira unazingatiwa ipasavyo. Kwa sababu hiyo, mpango wa FCPF umeamua kutumia taadhari katika awamu ya utayari wa MKUHUMI+ ambazo zinafuata matumizi ya Tathmini ya Kikakati ya Mazingira na Jamii (maarufu kama SESA) (Moss et al., 2011). SESA ufuata taratibu za uchambuzi na ushirikishwa katika maandalizi ya R-PP na R-Package (Moss et al., 2011). Zao kuu la SESA ni Mkakati wa Usimamizi wa Jamii na Management (ESMF), ambao ni mfumo wa kuepuka na/ au kupunguza na kusimamia uwezekano wa hathari za mikakati ya MKUHUMI+. Kwa kawaida, ESMF inapaswa kwendana na sera husika ya Benki ya Dunia na vile vile ESMF inapaswa kuwa na kipengele ambacho kinaelezea jinsi mahitaji ya sera husika yanavyoshughulikiwa.

Taadhari za MKUHUMI+ za Mkakati wa Umoja wa Mataifa Juu ya mabadiliko ya Hali ya Tabia Nchi (UNFCCC)

Maongezi juu ya taadhari za MKUHUMI+ yanafanyika kama sehemu ya majadiliano katika mazungumzo ya Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (UNFCCC) (Herbertson, 2011). Waraka wa UNFCCC unatoa wito kwa mataifa wanachama kuandaa na kutekeleza seti ya taadhari, ikiwa ni pamoja na zile zinazoshughulikia masuala ya kijamii ya utawala wa msitu, kuheshimu haki za wazawa na jamii husika, ushirikishwaji wa wadau pamoja na uimarishaji wa faida za kijamii (sanduku la 2); na kwa nchi zinazoshiriki katika mchakato wa MKUHUMI+ kuandaa mfumo wa kutoa taarifa juu ya taadhari zilizoandaliwa (UNFCCC, 2010:). Maamuzi mengine ya ziada katika mkutano huo UNFCCC wa 2011 ni makubaliano kwamba shughuli zote za MKUHUMI+ ni lazima ziongozwe na taadhari bila kujali chanzo cha fedha za kutekeleza shughuli hizo. (UNFCCC, 2011). Hata hivyo, bado hakuna makubaliano juu ya nini kipaumbele kati ya thamani za kikaboni dhidi ya zile zisizo za kikaboni za misitu na hivo viwango vya taadhari (McDermott et al 2012). Hali kadhalika, bado hakujakuwepo makabuliano juu ya vigezo vinavyofanya taadhari iwe kamilifu na pia haijulikani ni hatua gani zitachukuliwa endapo nchi itashindwa kuheshimu na kutekeleza mfumo wa taadhari.

Viwango vya Mazingira, Jamii na Bioanuwai

Viwango hivi vya Mazingira, Jumii na Bioanuwai (CCB) ulenga kuhakikisha kwamba mradi unatengeneza athari nyingi juu za kijamii na kiuchumi dhidi ya ustawi wa jamii husika ambazo ni zaidi ya ile dhana ya mradi kutokuwa na madhara kwa wananchi'—do no harm'. Viwango hivi vya CCB hutambua na kuthamini haya ya ushirikishwaji wa wananchi katika kubuni na kutekeleza miradi. Pia viwango usisitiza tathimini ya bioanuai kabla ya mradi pamoja na thamani ya shughuli za uhifadhi katika eneo la mradi. Kibali huru na taarifu pamoja na mfumo wa usawa wa ugawanaji mapato pia unahitajika.

Sanduku la 2: Taadhari za MKUHUMI+ chini ya Mkakati wa Umoja wa Mataifa UNFCCC

UNFCCC, katika waraka wa makubaliano wa Cancun ilielezea taadhari saba za jamii na mazingira zinazohusiana na MKUHUMI+ (UNFCCC, 2010). Hizi ni kama zifuatazo:

1. Matendo yachangia ama yaendane na malengo ya mipango ya taifa ya misitu pamoja na mikakati na makubaliano husika ya kimataifa
2. Mifumo wazi na halisia ya taifa ya usimamizi wa misitu, ambayo inazingatia sheria za nchi na uhuru wake
3. Kuheshimu ujuzi na haki za wazawa na wenyeji na jamii nzima za maeneo husika kwa kuzingatia vigezo/taratibu husika za kimataifa,hali halisi ya taifa husika na sheria zake,na pia kwa kuzingatia kwamba baraza kuu la Umoja wa Mataifa limepitisha waraka wa haki za wazawa.
4. Ushiriki yakinifu wa wadau husika, hasa wazawa na jamii nzima ya maeneo husika, katika shughuli zilizotajwa katika haya ya 70 and 72 ya waraka huu.
5. Kwamba shughuli ziendane na uhifadhi wa misitu ya asili na bioanuai, kwa kuzingatia kwamba shughuli zilizotajwa katika haya ya 70 hazitumiki kubadikisha misitu ya asili ila badala yake zinatumilka kama motisha ya kuifadhi misitu ya asili na huduma zitokanazo na mifumo ikolojia hiyo, na pia kuimarisha faida nyingine za kijamii na kimazingira.
6. Shughuli hizo zitatue matatizo ya mageuzi
7. Shughuli hizo zipunguze uhamishaji wa hewa ya ukaa

Sanduku la 2 linatoa mfano wa mradi ambao unatumia viwango vya CCBA katika nchi ya Tanzania.

Mifumo mingine ya Taadhari za MKUHUMI+

Mpango wa Taadhari za jamii na mazingira za MKUHUMI+ (REDD+ SES) ambao unaongozwa na Umoja wa viwango vya Mazingira Jamii na Bioanuwai (CCBA, ambaye ndiye mwanzilishi wa viwango vya mradi vya CCB) na CARE International, unalenga kuunganisha mashirika ya kiraia, na sekta binafsi pamoja na mashirika ya serikali katika kuandaa viashiria mahususi kwa nchi husika ili kuongoza mipango ya MKUHUMI+ ambayo inaongozwa na nchi husika zenyewe ili iendane na kanuni na vigezo vya mpango huo (CCBA & CARE, 2010).

Mpango wa UN-REDD umeandaa seti ya "kanuni na vigezo vya kijamii na kimazingira" kwa kutumia mfumo wa Umoja wa Mataifa wa haki za binadamu katika maendeleo (UN- REDD mpango, 2011). Mapungufu ya kanuni na vigezo hivi ni kushindwa kukosa rejea maalum katika maswala ya umiliki wa ardhi ambalo ni suala nyeti katika nchi zinazoendelea (Herbertson, 2011). Aidha, na kinyume na taadhari za FCPF na Benki ya Dunia, taadhari za UN-REDD hana utaratibu rasmi wa uwajibikaji. Tofauti hii katika taratibu za Umoja wa Mataifa na zile za Benki ya Dunia inasemekana kuleta changamoto katika nchi ambako mifumo yote miwili inatumika kwa pamoja (Baastel na Nordeco, 2011).

Mfuko wa Kijani wa mabadiliko ya tabia nchi (Green Climate Fund) ambao unatarajiwa kuwa mfumo ufadhili wa shughuli mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ikiwa ni pamoja na MKUHUMI+ (Ballesteros, 2011), ulianzishwa rasmi mwaka 2010, na ilizinduliwa rasmi mjini Durban, Afrika Kusini mwaka 2011. Benki ya Dunia alichaguliwa kama mdhamini wa mpito wa mfuko huu na bado majadiliano yanaendelea juu ya mpango wa taadhari wa Mfuko (Moss et al., 2011).

Sanduku la 2: Kuifanya MKUHUMI+ Inufaishe Jamii and Uhifadhi wa Misitu: Mradi wa Mfano wa TFCG kutoka Tanzania

Lengo la mradi huu ni kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa (kutokana na ukataji miti na uharibifu wa misitu) kwa njia ambazo zinatoa motisha ya moja kwa moja na ya usawa kwa jamii husika za vijijini ili kuhifahi na kusimamia misitu kiuendelevu. Mradi unalenga kujaribisha mfumo ambapo fedha/mapato ya MKUHUMI+ yanatumika kuongoza upunguzaji wa hewa ya ukaa kwa kutoa motisha moja kwa moja kwa jamii zenye misitu katika ardhi yao. Kwa kuzingatia ukosefu wa soko la kisheria la kaboni za MKUHUMI+ na pia ukosefu wa mfuko maalum wa kaboni hizo, mradi huu unalenga kuzisaidia jamii hizi kupata fedha kutoa masoko ya hiari ya kaboni (voluntary market)

Kwa mujibu wa Campesse (2011), mradi huu unalenga kuzingatia taadhari mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Katika ngazi ya kitaifa, mradi huu utazingatia mfumo wa sheria na taratibu za nchi. Hali kadhalika, mradi huu utafanyiwa tathmini na kuthibitishwa kwa kutumia Viwango vya Hiari vya Kaboni (VCS) pamoja na viwango vya Mazingira nchi, Jamii and Bioanuai (CCB).

Katika kutekeleza hili, mradi umekwisha kupata vibali huru na taarifu kutoka katika vijiji 36 vinavyoshiriki katika mradi huu. Mradi umeandaa mfumo wa uwazi na usawa juu ya maamuzi ya ugawanaji wa mapato yatokanayo na MKUHUMI+ na kuhakikisha kwamba jamii nzima inanufaika na mapato ya MKUHUMI+. Kwa mujibu wa MJUMITA and Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), ambao ndio mashirika mawili yasiyo ya kiserikali yanayotekeleza mradi huu, wameshirikiana na wanawake na wanaume kutoka katika kila kijiji katika kutambua mikakati inayofaa kutatua tatizo la uakataji miti na uharibifu wa misitu, na pia wamefanya tathimini shirikishi ya jamii katika ngazi ya kijiji na mradi. Pia wanashirikiana na jamii husika kutekeleza 'mipanga' iliyoandaliwa. Sambamba na shughuli hizi,mashirika haya yamekuwa yakifanya pia shughuli za kitaalamu zaidi zinazohusiana na maswala ya MRV na kundaa maandiko ya kifundi ya mradi (PDD) kwa ajili ya tathimini za VCS na CCB. Tathimini ya Kaboni pia imekwisha fanyika kwa kushirikiana na wanajamii. Matokeo ya uchambuzi wa mabadiliko ya msitu yameingizwa katika mpango shirikishi ya matumizi ya aridhi pamoja na mpango shirikishi wa usimamizi wa misitu. Pia, mfumo wa ufuatiliaji wa bioanua katika maeneo ya mradi umeandaliwa.

2. UTEKELEZAJI WA TAADHALI ZA MKUHUMI+ KATIKA AFRIKA MASHARIKI

Sera Zilizopo na Maendeleo yaliyofikiwa

Kwa upande wa maendeleo katika kutekeleza shughuli za MKUHUMI+, Tanzania inasemakana kuwa hatua moja mbele ya Uganda na Kenya. Kenya na Uganda zimewasilisha R-PPs zake katika Benki ya Dunia-Ushirika wa Kaboni ya Misitu (GoK, 2010;GoU 2011), wakati Tanzania imekamilisha rasimu ya pili ya mkakati wa taifa wa MKUHUMI+ (URT, 2012). R-PP inatoa tathmini na taswira ya mwenendo wa mapana wa matumizi ya ardhi, visababishi vya moja kwa moja ama vinginevyo vya ukataji miti na uharibifu wa misitu katika sekta zote muhimu, pamoja na masuala muhimu zaidi yanayohusiana na umiliki wa ardhi, haki za maliasili na masuala muhimu ya utawala. R-PPs pia zinaonyesha mafanikio na vikwazo vya jitihada zilizopita katika kutekeleza sera au hatua kwa ajili ya kushughulikia visababishi vya ukataji miti na uharibifu wa misitu, na kubainisha mapungufu muhimu, changamoto pamoja na fursa za kutekeleza MKUHUMI+. Tathmini hii inapaswa kutoa mwanya kwa ajili ya kuandaa mkakati wa taifa wa MKUHUMI+ kwa ajili ya kushughulikia visababishi vikuu vya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

Tanzania

Mkakati wa Taifa wa MKUHUMI+ nchini Tanzania, unatambua kwamba sera na mfumo muhafaka wa kisheria ni muhimu kwa ajili ya kutekeleza shughuli za MKUHUMI+. Rasimu ya pili ya Mkakati wa Taifa wa MKUHUMI+ nchini Tanzania (URT, 2012) inazingatia sera na sheria husika mbalimbali ambazo ni muhimu ili kuhakikisha kwamba ustawi wa jamii pamoja na hoja nyingine za mazingira zinashughulikiwa ipasavyo. Mkakati unabainisha kwamba Tanzania inatarajia kuandaa utaratibu wa wazi wa taadhari za MKUHUMI+ kufikia mwezi Desemba 2012 (URT, 2012). Jitihada tayari zinaendelea ili kujenga uwezo juu SESA katika ngazi za kitaifa na katika serikali za mitaa, na pia kushughulikia mambo ambayo yanaweza kuwa vikwazo vya mafanikio ya MKUHUMI+.

Mkakati wa taifa wa MKUHUMI+ unabainisha dhamira ya kuhakikisha kwamba thamani ya bioanuai ya taifa na mifumo ikolojia ya misitu inahifadhiwa na kuboreshwa, na kwamba, faida, mapato na huduma zitokanazo na rasilimali hizo yanagawanywa kwa usawa miongoni mwa wadau wote ili kusaidia katika kuhimili na

kuzuia mabadiliko ya tabia nchi lakini pia katika kuweza utekelezaji wa dhana ya kufikia mendeleo kupitia njia ya kaboni kidogo kama inavyotakiwa na UNFCCC (URT, 2012). Mkakati huu pia unabainisha hatari - za ndani na nje- ambazo zinaweza kuikumba nchi katika mchakato wa kutekeleza mkakati wake wa MKUHUMI+. Kulingana na URT (2012), hatari ni pamoja na ukosefu wa vyanzo mbadala na nafuu ya nishati katika kipindi cha mpito, uwezekano wa kuhamishia sehemu nyingine shughuli za ukataji miti, kuwanyima ama kuwapunguzia wananchi upatikanaji wa misitu kwa ajili ya shughuli ndogo ndongo za kilimo kwa wakulima ama kwa ajili ya nishati mathalani kutokana na sababu kwamba jamii hiyo haina umiliki halali wa msitu, ama kutokana na ushurikishwaji mdogo wa jamii katika shughuli za MRV kutokana na changamoto ambazo zinayakumba maswala ya MRV, pamoja na wasomi kuwapokonya maskini mashamba yao yenye miliki za kimila ambazo wakati mwingine ni vigumu kuthibitisha kisheria.

Kama hatua ya kushughulikia hatari hizo, mkakati huo unaonyesha kwa mfano, kwamba shughuli zote za MKUHUMI+ itabidi zifanyike sambamba na malengo ya programu ya Taifa ya Misitu, bila kukiuka haki za jamii-tegemezi za misitu pamoja na wazawa, hasa kutokana na ukweli kwamba Tanzania imeridhi Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Wazawa, na kuhakikisha uhusishwaji kamili wa wadau husika. Aidha, mkakati unasisitiza utekelezaji wake utafanyika kulingana maelekezo na matakwa ya SESA kwa mujibu wa, miongoni mwa mambo mengine, sera na kanuni za mazingira zilizopo pamoja na taadhari za Benki ya Dunia.

Kuna idadi kubwa ya sera na sheria ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa MKUHUMI+ nchini Tanzania. Hizi ni pamoja na Dira ya Taifa ya maendeleo ya 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Sera ya Taifa ya Mazingira (1997), Sera ya Misitu (1998) na Sera ya Ardhi (1995). Sera zote hizi zinalenga kuhakikisha kwamba rasilimali za misitu zinahifadhiwa na kutumika katika njia endelevu ili kupunguza umaskini hasa wa jamii zinazoishi karibu na misitu. Sera nyingine ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa MKUHUMI+ ni Sera ya Taifa ya Nishati na Kilimo na Sera ya Mifugo (1997).

Uganda

Uganda imewasilisha R-PP kaitika Ushirika wa Kaboni ya Misitu wwa Benki ya Dunia (FCPF), lakini bado Uganda haijaandaa mkakati wa taifa MKUHUMI+ mkakati. Shabaha kubwa ya uandaaji wa taadhari za MKUHUMI+ kwa Uganda inalenga SESA. Serikali inalenga kuhakikisha kwamba shughuli zote za MKUHUMI+ zinazingatia sheria na sera zilizopo. Kuna mambo mbalimbali katika sheria zilizopo ambayo yatasaidia katika kuandaa SESA ya MKUHUMI+. Kwa mfano, uadaaji wa sera ya Taifa ya Misitu (2001) uliongozwa na kanuni zifuatazo ambazo kwa ujumla zinalenga vipaumbele vya serikali juu maendeleo ya taifa, kuondoa umaskini na utawala bora:

i. Malengo ya Taifa: Sera ya Misitu inaendana na kanuni za jumla zinazolenga maendeleo endelevu ambazo zinapatikana katika Katiba na Dira 2025.
ii. Huifadhi na maendeleo endelevu: Misitu ya Uganda inapaswa kuhifadhiwa ili kukidhi mahitaji ya kizazi cha sasa bila kuathiri haki za vizazi vijavyo.
iii. Ustawi wa jamii na umaskini: uboreshaji wa maisha ya watu ndio linapaswa kuwa lengo kuu katika mikakati yote ya maendeleo ya sekta ya misitu, ili kuchangia katika kutokomeza umaskini.
iv. Bioanuwai na huduma za mazingira: maendeleo ya sekta ya misitu yanapaswa kulinda bioanuai za taifa za msitu pamoja na huduma za mazingira kupitia mikakati madhubuti ya uhifadhi.
v Ushirikiano katika utawala: Ushirikiano/mahusiano mapya ya kitaasisi hayana budi kuongeza ufanisi, uwazi, uwajibikaji na ueledi, na hivo kujenga imani kwa wadau wote wa misitu.
vi. Jinsia na usawa: kuhakikisha ushiriki wa watu wote na matendo ya usawa ya kijinsia dhidi ya wanawake wote, vijana, vikundi wazee na makundi dhaifu au wasiojiweza katika maendeleo ya sekta.
vii. Utamaduni na taasisi za kijadi: maendeleo ya sekta misitu yanapaswa kuzingatia utamaduni na taasisi jadi.
viii. Wajibu wa Kimataifa: sheria inabidi ziandaliwe ili kusaidia utekelezaji wa ahadi za kimataifa zilizopo sasa na zile zijazo ambazo zinahusu sekta ya misitu.
ix. Uthamini wa Misitu: thamani za kimazingira na kijamii zinapaswa kutumika katika kutathimini gharama na faida wakati kwa ajili ya kuandaa mikakati ya kutekeleza Sera ya Misitu

Sanduku la 3: Kushindwa kwa Taasisi na Ukosefu wa Uwezo-Kikwazo katika utekelezaji wa taadhari: Somo kutoka katika sekta ya nishati nchini Uganda

Uganda inazo sheria na sera kadhaa ambazo zinalenga kuwakinga watu na mazingira dhidi ya hatari. Hizi ni pamoja, kwa mfano, sheria juu ya upatikanaji wa habari/taarifa, usalama wa wafanyakazi, kuzuia uchavi wa mazingira na kuthani urithi wa utamaduni. Wakati sera na sheria hizi ziko wazi katika makaratasi, mara nyingi zimekuwa hazitekelezwi kama inavyotakiwa (Herbertson, 2012). Hii imepelekea matatizo ya kijamii na kimazingira ambayo yamewahi kuripotiwa na mashirika ya kiraia katika shughuli za uandaaji na ujenzi wa mabwawa ya umeme wa maji.

Ugunduzi wa mafuta nchini Uganda mwaka 2006 umevutia wawekezaji binafsi wa kimataifa ambao wanashinda kupata ya malimbikizo hayo ya mafuta. Zaidi ya visima 60 tayari vimekwisha kuchimbwa hadi sasa ambapo uchunguzi wa Henry Mugisha Bazira wa Water Governance Institute maendeleo haya hayaongozwi kabisa na sera husika za taadhari (Bazira, 2012). Uchunguzi huu ulionyesha kwamba ni kampuni moja tu ya Tullow Oil, ambayo imejitolea kutumia viwango vya ufanisi vya International Finance Corporation. Madhara ya kimazingira na kijamii yatokanayo na maendeleo haya yanapaswa kushughulikiwa na mamlaka na sheria husika. Hata hivo, na kama ilivokwisha kutajwa hapo juu, mamlaka hizi ni adha dhaifu, zinatekelezwa chini ya kiwango au hazipo kabisa. Serikali ya Uganda iko kwa hivi sasa katika mchakato wa kuandaa sheria na taasisi muhimu kwa ajiri ya kusimamia sector ya mafuta,ila bado rushwa na matatizo ya kitaasisi yanaathiri mchakato (Bazira, 2012).

Mara nyingi majadiliano kati ya serikali na makampuni ya mafuta yanafanyika kati vyumba vilivofungwa dhidi ya uma na wanasiasa. Kuna miradi ambayo inendelea kutekelezwa katika ukanda wa Albertine Graben; ukanda ambao umeteuliwa kuwa kitovu cha bioanuai; ila bado serikali haijakubali kuweka wazi ripoti za tathmini za mazingira za miradi hiyo inayoendelea. Wananchi katika eneo lile hawafahamu chochote kuhusu miradi hiyo na tayari ripoti zimekwishatolewa juu ya unyanganyi wa aridhi. Kwa mujibu wa Bazira (2012), ugunduzi wa mafuta umeibua hisia tofauti miongoni mwa wananchi wa Uganda. Kwa upande ukuaji wa kiuchumi unategemewa wakati kwa upande mwingine changamoto ni dhahiri ambazo mfumo wa utawala wa serikali hauna hatua madhubiti za kuchukuliwa katika kushughulikia uharibifu wa kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Aidha, sehemu ya 38 ya sheria ya Taifa ya Misitu na Upandaji Miti (2003) inamtaka mtu yeyote mwenye dhamira ya kufanya mradi au shughuli, ambayo inaweza, au ina uwezekano mkubwa wa na athari kubwa katika mazingira, kufanya tathimini ya madhara ya mazingira (EIA). EIA hiyo inapaswa kufanyika kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Taifa ya Mazingira (NEA, 1995). Orodha ya 3 ya NEA inaeleza wazi miradi ambayo inahitaji EIA na hii ni pamoja na shughuri zinazohusiana na mipango ya MKUHUMI+ kama vile kama vile urejeshaji miti na upandaji miti..

Kenya

Kama Uganda, Kenya bado haijaandaa mkakati wa taifa wa MKUHUMI+. Hata hivyo, haja ya kuandaa taratibu za taadhari ili kulinda na kushughurikia athari kwa wadau katika nafasi ili kuzuia au kudhibiti athari mbaya kwa wadau kutoka kutokana na shughuri za MKUHUMI+ imewekwa wazi kwenye R-PP. Taratibu za kutekeleza SESA zimeeezwa katika R-PP na mashauriano yaliyoko katika R-PP yanatarajiwa kujumuishwa vilivyo katika mchakato wa jumla wa mashauriano juu ya R-PP. Athari za kimazingira na kijamii zinazoweza kutokana na shuguri zilizopangwa, zinatarajiwa kushughurikiwa kupitia mashauriano na wadau ambapo namna na fursa za kuzishughurikia zitatambulika.

Wakati wa mchakato wa uandaaji wa R-PP, watu zaidi ya 200, wakiwakilisha makundi muhimu ya wadau kuu ikiwa ni pamoja na vikundi vya jamii kutoka msituni na makundi ya watu asilia, walihusika katika zaidi ya moja ya hatua za mchakato huo. Wakati wa mashauriano na wadau mbalimbali, masuala ya kijamii na mazingira yalijadiliwa pamoja na matarajio ya wadau, majukumu, na wajibu wao katika kuandaa mkakati wa taifa wa MKUHUMI+. Miongoni mwa matokeo ya mashauriano hayo ni taarifa ya wito wa jumuiya ya jamii tegemezi za misitu 'kutaka kuhakikishiwa kwamba mpango wa

MKUHUMI+ hautawanyika haki yao ya ardhi na pia kuwanyika haki ya kupata mazao ya misitu (Gok, 2010)

Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira ya Sera ya Misitu ya Kenya ulifanyika mwaka 2005 na matokeo yake yanatarajiwa kuwa msingi tathmini za kijamii na kimazingira katika shughuri za MKUHUMI+. Aidha,shughuli za MKUHUMI+ zitatakiwa kuzingatia sheria ya nchi ya mazingira ambayo inatambua na kuzingatia kanuni na dhana za kisasa za usimamizi wa mazingira kama vile ushiriki wa umma, ushirikiano wa kimataifa, kanuni za tahadhari, pamoja na kanuni za jadi za kijamii na kiutamaduni ambazo utumiwa na jumuiya yoyote nchini Kenya kwa ajili ya usimamizi wa maliasili.

Zipo sera na sheria ambazo ni sambamba na ulinzi wa kijamii na kimazingira katika mukitadha wa MKUHUMI+. Kwa mfano, Kenya "Dira 2030" ina sehemu ambayo inahusiana na kubadilisha na kuboresha mandhari ya msitu. Sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira (EMCA, 1999) inalenga kuoanisha mbalimbali sheria mbalimbali za kisekta ambazo zinagusa mazingira ili kuleta ufanisi mkubwa katika kuhifadhi mazingira ya asili na yale ya kijamii. EMCA inatoa mfumo kwa kuunganisha masuala ya mazingira katika shughuri zote za kimaendeleo, kiuchumi na kijamii.

Kenya pia ina vigezo na viashiria kwa ajili ya usimamizi endelevu wa misitu ambavyo vinatarajiwa kuchangia katika kuunda seti madhubuti kina ya taadhari za kijamii na mazingira kwa ajili ya kutekeleza shughuli za MKUHUMI+.

© Adrian Paul Nel

3. KUFANIKISHA TAADHARI ZA MKUHUMI+ KATIKA AFRIKA MASHARIKI

Miongozo kutoka kwa Washiriki katika Warsha juu ya Masuala ya Taadhari za MKUHUMI+

Ili ziweze kufanya kazi, taadhari hizi itabidi ziwe mahususi kwa sehemu na mahala husika, hali ambayo inaashiria umuhimu wa kuwa na taasisi husika katika kila ngazi. Taadhari ambazo ni mahususi kwa sehemu huzika inabidi ziandaliwe ili kuboresha zile za kimataifa. Kwa hiyo taratibu mahusi kwa kila sehemu/mradi zinahitajika. Kama za vijiji zaweza kuwa sehemu nzuri ya kuanzia.

Mashirika ya kiraia yana mchango mkubwa katika kufanikisha taadhari husika kwani yana mahusiano ya moja kwa moja na jamiii husika. Kwa mfano, MJUMITA kutoka Tanzania, Mtandao wa Jumuiya ya Vyama Misitu nchini Uganda (UNETCOFA) na Muungano wa Kitaifa wa Vyama Misitu ya Jamii wa Kenya, yanamchango muhimu sana. Kinachohitajika ni uwezeshwaji, na wala sio tu ushiriki.

Mawasiliano yanapaswa kuwa sehemu muhimu ya taadhari. Jamii zinapaswa kufahamu lakini pia wafadhili wanapaswa kutambua mahitaji ya ili MKUHUMI+ iweze kufanikiwa Ueleweshaji juu ya taadhari za MKUHUMI+ unapaswa kufanywa na watendaji ambao wanaelewa vizuri mada na pia wanaweza kuwasilisha inavyotakiwa.

MRV juu ya taadhari isiwe tu kwa ajili ya wafadhiri, bali pia kwa jamii na wadau wengine. Ushiriki wa jamii katika utekelezaji na kutoa taarifa juu ya taadhari ni jambo linalowezekana ili mradi tu kuwepo na mawasiliano na ufahamu.

Ilionekana pia kwamba rushwa itaathiri utekelezaji wa MKUHUMI+ na hivo mashirika ya kiraia - na watendaji wengine wa MKUHUMI+- wanapaswa kuangalia swala hii kwa umakini zaidi. Umuhimu wa haja ya mbinu muhafaka za kushughurikia swala hili ulitiliwa mkazo. Na kwa sababu hiyo, taadhari pekee hazitatosha bila kutolewa fursa na foramu za kujadili na kushughurikia vyanzo vya rushwa.

Nchi za Afrika Mashariki zinaweza kuangalia namna ya kuoanisha taadhari za ili kuhimalisha na kufanikisha utawala bora na uwajibikaji. Ilionekana kwamba uoanishaji wa taadhari unawezekana endapo nchi Afrika Mashariki itaamua hivyo, lakini pia kunaweza kuhitajika mwanzilishi wa jambo hili ambapo mashirika ya kiraia

yana nafasi nzuri ya kufanya hivi.

Pia wasiwasi uliibuka miongoni mwa washiriki juu ya dhana ya nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki.Kwamba, badala ya kutekeleza sera ya mabadiliko ya tabia nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo tayari ipo na pia Mipango kazi ya pamoja, nchi za Afrika Mashariki zimeendela kuandaa mikakati binafsi ya kitaifa ambayo haizingatii sera hii ya kikanda—yaani zinadi kujitenga na muungano.

Utekelezaji fanisi wa taadhari utaambana na gharama na kwa hiyo, kuna haja ya kuanda fungi kwa ajili ya gharama hizi za awali hasa kwa wajamii.

Daima, MKUHUMI+ utapata usikivu na mapokeo ya kutosha kulingana na jinsi wanasiasa watakavyoupokea. Kuna, kwa hiyo, haja ya dhamira ya kisiasa kutekeleza ulinzi.

REDD + ulinzi inapaswa kufanya kazi kwa njia ya miundo ya ndani lakini haya ni katika baadhi ya kesi haupo. Hivo basi kuna haja ya kuhakikisa kuna mwitiko wa kisiasa katika kutekeleza taadhari za MKUHUMI+.

Utekelezaji wa taadhari za MKUHUMI+ unapaswa kufanyika kupitia katika miunda na taasi za jamii husika, lakini miundo hii pengine haipo sehemu nyingi. Hivo, hatua ya kwanza inabidi iwe ni kuandaa taasisi husika.

Kwa kuangalia katika haki za jamii juu ya rasilimali, kuna haja ya kuzingatia uvunjaji wa utaratibu kama kuvamiwa kwa rasilimali hizo.

Taadhari hazipaswi kuwa sentensi tupu na nadharia bali mambo ambayo yanaweza kufanyika na kuwa na matokeo halisia kwa watu. Taadhari zisiwe kwa ajili ya Umoja wa Mataifa bali kwa ajili ya jamii husika. Isiwe tu uandaaji wa taadhari bali muhimu zaidi utekelezaji.

Umuhimu wa kuangalia sheria na sera ambazo tayari haupaswi kupuuzwa. Miradi ya majaribio pia ni sehemu muhimu pia kujifunzia. Wasiwasi juu ya Sera husiwe hasa kuhusu kufafanua sera / mbinu zitakazotumika bali muhimu zaidi kuhusu utekelezaji na kuhakikisha kwamba masomo kweli yanajifunzwa.

© Adrian Paul Nel

4. HITIMISHO

Uchambuzi wa sera na mifumo ya kisheria iliopo unaonyesha kwamba taadhari za MKUHUMI+ sio dhana mpya katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, kuna mapungufu muhimu, pamoja na changamoto katika utekelezaji, ambayo yanahitaji kushughulikiwa.

Taadhari za MKUHUMI+ zinapaswa kuunganishwa katika michakato ya kitaifa kwa vile hii uleta uepesi wa kufafanua taadhari kulingana na masuala ya muhimu ya kitaifa au kulingana na mifumo iliyopo. Hata hivo, ni muhimu kuhakikisha kwamba taadhari za ngazi ya taifa zinaendana na viwango vya taadhari za kimataifa.

Kuna uwezekano mkubwa wa rushwa na mazingira ya kisiasa kuathiri sana utekelezaji wa taadhari za MKUHUMI+. Asasi za kiraia na sekta binafsi zinapaswa kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza taadhari hizi. Vyama vya misitu ya jamii na mashirika ya mazingira havina budi kuweza ili kusimamia jambo hili.

Ushiriki wa jamii na mashauriano nao ni jambo muhimu. Jamii zinapaswa kuelemishwa kuhamasishwa vya kutosja kuhusu MKUHUMI+ na taratibu zake ili kuhakikisha zinashiriki kikamilifu.

Taadhari za MKUHUMI+ ziwe kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya wafadhili au kuonyesha utimizaji wa matakwa ya kimataifa, bali kuhakikisha ustawi wa jamii na mazingira na utoaji bora wa matarajio ya MKUHUMI+.

Kuna haja ya uongozi wa kisiasa kuonyesha dhamira na utashi wa kutekeleza sera na sheria ili kuepuka taadhari za MKUHUMI+ kuishia kwenye karatasi kama sera nyinginezo.

References

Baastel and Nordeco (2011) First Program Evaluation for the Forest Carbon Partnership Facility, Prepared for the FCPF Participants Committee. Available at: http://www.forestcarbonpartnership.org/fcp/sites/forestcarbonpartnership.org/files/Documents/PDF/Jun2011/5.%20Final%20FCPF_EVALUATION_REPORT_June%2013th.pdf

Ballesteros, A. (2011) The Road to the Green Climate Fund. World Resources Institute. Available at: http://www.wri.org/stories/2011/02/road-green-climate-fund.

Bazira H. M. (2012) Uganda's Civil Society Perspectives on International Reforms of Environmental and Social Safeguards for Development Finance. Water Governance Institute.

Bonfante, T.M., Voivodic, M. & Meneses Filho, L. (2010) Developing social and environmental safeguards for REDD+: A guide for a bottom-up approach http://www.imaflora.org/upload/repositorio/guiaREDD_ingles_digital.2.pdf

Campese, J. (2011) Integrating REDD+ Social and Environmental Safeguards and Standards in Tanzania . TFCG Technical Report 32. Pp 1 - 65. Dar es Salaam.

CCBA and CARE (2010) REDD+ social & environmental standards. Version 1. Jun 2010. Climate, Community & Biodiversity Alliance and Care International, Washington, DC and Nairobi, Kenya. Available at: http://www. cbd.int/doc/meetings/for/wscbredd-afr-01/other/wscbredd-afr-01-socenv-en.pdf.

Danielsen et al (2011) At the heart of REDD+: a role for local people in monitoring forests? Conservation Letters 00 (2011) 1-10 http://unfccc.int/files/methods_science/redd/application/pdf/redd_heart_paper2011.pdf

Dkamela, G.P. (2011) The context of REDD+ in Cameroon: drivers, agents and institutions. Occasional paper 57. CIFOR, Bogor, Indonesia. 63p.

GoK (2010) Revised REDD Readiness Preparation Proposal for Kenya. Submitted to the Forest Carbon and Partnership Facility. Government of Kenya.

GoU (2011) REDD Readiness Preparation Proposal for Uganda. Submitted to the Forest Carbon and Partnership Facility. Government of Uganda.

Herbertson K. (2012) Will Safeguards Survive the Next Generation of Development Finance? International Rivers.

Jagger, P., Lawlor, K., Brockhaus, M., Gebara, M. F., Sonwa, D. J. and Resosudarmo, I. A. P. (2012) REDD+ safeguards in national policy discourse and pilot projects. In: Angelsen, A., Brockhaus, M., Sunderlin, W.D. and Verchot, L.V. (Eds) Analysing REDD+: Challenges and choices. CIFOR, Bogor, Indonesia.

May, P.H., Millikan, B. and Gebara, M.F. (2011) The context of REDD+ in Brazil: drivers, agents, and institutions. CIFOR, Bogor, Indonesia. 69p.

McDermott, C.L., Coad, L., Helfgott, A., Schroeder, H. (2012) Operationalising social safeguards in REDD+: actors, interests and ideas. Environmental science and policy 21: 63 - 72

Moss, N., Nussbaum, R., Muchemi, J. and Halverson, E. (2011) A Review of Three REDD+ Safeguard Initiatives. A study commissioned by the UN-REDD programme and the Forest and Carbon Partnership Facility.

Murphy, D. (2011) Safeguards and multiple benefits in a REDD+ mechanism. International Institute for Sustainable Development, Winnipeg, Canada. 37p.

UNFCCC (2010) The Cancun Agreements 1/CP.16. United Nations Framework Convention on Climate Change.

UNFCCC (2011) Outcome of the work of the Ad Hoc Working Group on Long-term Cooperative Action under the Convention. 2/CP.17. United Nations Framework Convention on Climate Change

UN-REDD Programme (2011) UN-REDD Programme Social and Environmental Principles and Criteria. Version 3 - draft for consultation. September 2011. The United Nations Collaborative Programme on Reducing Emissions from Deforestation and Forest Degradation in Developing Countries. Available at: http://www.un-redd.org/Multiple_Benefits_SEPC/tabid/54130/Default.aspx.

URT (2012), National Strategy For Reduced Emissions From Deforestation And Forest Degradation (REDD+) June, 2012. United Republic of Tanzania.

World Bank (2011) Forest Carbon Partnership Facility (FCPF) Readiness Fund Common Approach to Environmental and Social Safeguards for Multiple Delivery Partners.